Sunna za udhu

1.Kuosha vitanga viwili vya mikono mara tatu mwanzo wa kutawadha.

2.Kupiga mswaki.

3.Kuosha viungo mara tatu tatu, isipokuwa kichwa na masikio mawili, kwani hivyo havioshwi isipokuwa mara moja.

4.Kuanzia kuliani: nako ni kuanza upande wa kulia katika kuosha viungo vya udhu.

5.Kurefusha vingaja: yaani kupitisha zaidi ya vifundo vya mikono katika kuosha.

6.Kutoa mwanya kwenye ndevu ili kufikisha maji kwenye ngozi ya uso.

6.Kufikisha maji baina ya vidole vya mikono na miguu.

8.Kusugua viungo kwa mkono, na haitoshi kunyunyiza maji.

9.Kutumia maji kwa kiasi, kwa kuwa mtume ﷺ: amesema (Kutakuwa na watu katika umma huu watakaopitisha kiasi katika kujitwahirisha) [Imepokewa na Abu Daud.] Yaani watatumia maji ya kutawadhia kwa kupita kiasi

10.Dua baada ya kutawadha. Mtume ﷺ alisema: (Hakuna yoyote miongoni mwenu atakayetawadha, akaeneza maji ya kutawadhia kwenye viungo, kisha akasema “Nakiri kwa moyo kibaini kwa ulimi kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa mungu moja na Muhammad ni mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Ewe Mola! Nijaalie niwe miongoni mwa wenye kutubia na unijaalie ni miongoni mwa wenye kujitwahirisha” isipokuwa atafunguliwa milango ya pepo minane, auingie autakao) [Imepokewa na Tirmidhi.].

11.Kuswali rakaa mbili baada ya kutawadha. Mtume ﷺ alisema: (Mwenye kutawadha kama hivi ninavyotawadha, kisha akainuka akaswali rakaa mbili bila kusema na nafsi yake, atasamehewa dhambi zake zilizotangulia) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

https://www.al-feqh.com/sw/kutawadha

al-feqh.com/sw